

# Makosa ya Kisemantiki Katika Maandishi ya Wanafunzi Wageni Wanaojifunza Lugha ya Kiswahili.

**Mwanaidi Juma Jaku.**

*Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (Suza), Zanzibar, Tanzania*

*[jakumwanaidi@gmail.com](mailto:jakumwanaidi@gmail.com)*

---

*Received: April 2022, Accepted: June 2022, Published: December 2022*

*© SUMAIT University Journal 2022*

---

## **Abstact**

There have been a large number of students learning Swahili language in the world, this situationa caused by the development of science and technology including the rapid growth of the Swahili language in the world. During learning, various errors may arise. This article aims to explain semantic errors in the writings of foreign students learning Swahili language as well as the sources of those erroes. In this article documentary review and interview are the techniques used in data collection whereas the total of 24 students from The State University of Zanzibar (SUZA) and The Kiswahili na Utamaduni (KIU) centre were collected, and the total of 4 teachers were interviewed from those two centres, the author went direct to the field so as to collect those data. The data obtained were analyzed using descriptive approach and the observation revealed that there are a lot of semantic errors that happen in the writings of the foreign students learning Swahili language that are from different sources. Such errors include misuse of verb conjugation, the use of inappropriate vocabulary in the context, word-for-word separation, sound dropping, literal translation, word dropping, word linking and phonetic modification. And the sources being the effects of the first language, the difficulty of the second language rules and the lack of exposure among the students.

Therefore, based on those findings the author has suggested appropriate methods that wili help both the teachers and the stundents to identify the errors and their sources and work on them.

---

## **Ikisiri**

*Kumekuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili duniani, hali inayosababishwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia ikiwa ni pamoja na kukua kwa kasi kwa lugha ya Kiswahili duniani. Katika kujifunza huko makosa mbalimbali yanaweza kujitokeza. Makala hii ina lengo la kufafanua makosa ya kisemantiki katika maandishi ya wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili pamoja na vyanzo vya makosa hayo. Katika makala hii mbinu za udurusu wa nyaraka na usaili ndizo zilizotumika katika ukusanyaji wa data ambapo jumla ya kazi 24 za wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Kituo cha Kiswahili na Utamaduni (KIU) zilikusanywa, na jumla ya walimu wanne kutoka katika vituo hivyo walihojiwa, mwandishi alikwenda moja kwa moja uwandani ili kukusanya data hizo. Data zilizopatikana zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaeezo; na uchunguzi umebaini kuwa yapo makosa*

---

---

## Makosa ya Kisemantiki Katika Maandishi ya Wanafunzi Wageni Wanaojifunza Lugha ya Kiswahili, Mwanaidi Juma Jaku

---

*mbalimbali ya kisemantiki yanayojitokeza katika maandishi ya wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili ambayo yanatokana na vyanzo tafauti. Makosa hayo ni pamoja na matumizi mabaya ya mnyambuliko wa hali za vitenzi, matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha wake, kutenganisha neno pasipostahiki, udondoshaji wa kitamkwa katika neno, makosa ya tafsiri sisisi, udondoshaji wa maneno katika sentensi, kuunganisha maneno na kubadili mpangilio wa fonimu. Na vyanzo vikiwa ni athari ya lugha mama, ugumu wa sheria za lugha ya pili na ukosefu wa mazoezi miongoni mwa wanafunzi. Hivyo, kutokana na matokeo hayo mwandishi amependekeza mbinu sahihi zitakazowasaidia walimu na wanafunzi kugundua makosa pamoja na vyanzo vya makosa hayo na kuyafanyia kazi.*

---

**Key words:** makosa, semantiki, makosa ya kisemantiki

---

### 1.0 Utangulizi

Aruba (2017) amezungumzia makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili katika Kaunti ya Kakamega.

Aladin, Darus na Rajab (2016) wameandika kuhusu uchunguzi wa makosa ya kisemantiki katika maandishi kwa wanafunzi wa Libya wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya kigeni. Al- Shohbani na Al- Shormani (2012) walifanya utafiti kuhusu makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wa Vyuu Vikuu vya Yemen: Mgawanyo na vyanzo. Nao Ahmed na Zribi (2002) wamefanya utafiti kuhusu ugunduzi wa makosa ya kisemantiki katika maandishi ya Kiarabu.

Jeptarus na Ngene (2016) wamefanya utafiti kuhusu makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wa darasa la saba wanaozungumza lugha ya Keiyo wanapojifunza Kiswahili.

Kama ilivyoielezwa, lengo la makala hii ni kufafanua makosa ya kisemantiki katika maandishi ya wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili sambamba na vyanzo vyake. Matokeo ya makala hii kutoka nyanjani yamebaini makosa mbalimbali kutoka kwa wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili na vyanzo vya makosa hayo.

Kufuatia kuwepo kwa ongezeko kubwa la wajifunzaji wa Kiswahili duniani, vituo mbalimbali vya kufundisha Kiswahili vilianzishwa. Kwa upande wa Tanzania bara Kiswahili kilianza kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika miaka ya 1960 kitengo cha Kiswahili kwa wageni cha idara ya Kiswahili ndicho kilichokua na jukumu la kufundisha Kiswahili. Mwaka 2009 kitengo hiki kilibadilishwa na kuwa Kituo cha Kiswahili kwa wageni kilichokuwa chini ya uratibu maalumu. ([www.udsm.ac.tz/the-centre-for-kiswahili-for-foreigners](http://www.udsm.ac.tz/the-centre-for-kiswahili-for-foreigners)).

Na kwa Zanzibar, Kiswahili kama lugha ya kigeni kilianza kufundishwa mnamo miaka ya 1979 ikiwa chini ya usimamizi wa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (TAKILUKI) kwa wakati huo. Mnamo mwaka 2012 Kiswahili kama lugha ya kigeni kikawa rasmi chini ya Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni katika Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (SUZA). ([www.suza.ac.tz/school-of-kiswahili-foreignlanguage-skfl/](http://www.suza.ac.tz/school-of-kiswahili-foreignlanguage-skfl/)).

Corder (1987) anasisitiza kuwa makosa ni jambo lisilo epukika katika kujifunza lugha, makosa ndio yanayomuonesha mwalimu ni jinsi gani mwanafunzi ameelewa au hakuelewa kile alichojifunza. Hivyo, mwalimu anatakiwa kuchunguza makosa hayo, sababu zake na kujua njia sahihi za kuweza kuyarekebisha makosa hayo.

## 2.0 Makosa ya Kisemantiki

Mwandishi amegundua makosa mbalimbali ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wageni wanaojifunza Kiswahili, makosa hayo ni kama yanavyoelezewa hapo chini:

### 2.1 Matumizi mabaya ya mabadiliko ya hali za vitenzi

Kumekuwa na makosa kadhaa yanayotokana na matumizi mabaya ya kauli mbalimbali za vitenzi miongoni mwa wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili, miongoni mwa kauli hizo ni kauli ya kutendea, kutenda, kutendwa na kauli ya kutendesha.

#### 2.1.1 Hali ya kutendea

Katika aina hii ndogo ya makosa mwanafunzi ametumia hali za kutenda na kutendewa badala ya hali ya kutendea kama invyoonekana:

1. Kwa hivyo, watu wengi wanaotoka Ujerumani Mashariki **walikimbia** Ujerumani Magharibi.
2. Samahani naomba posti kadi sita **kupeleka** rafiki wangu.
3. Joyce **anafunguliwa** John mlango.
4. Wakati wa jioni Lucas hupenda **kutembelewa** Forodhani.

Katika sentensi (1) mwanafunzi ametumia neno **walikimbia** ambalo linaonesha hali ya kutenda badala ya neno **walikimbilia** na hivyo kubadili maana iliyokusudiwa.

Neno **kupeleka** katika sentensi (2) limetumika kuonesha hali ya kutenda badala ya neno **kupelekea** ambalo ni hali ya kutendea na kusababisha kupotosha maana iliyokusudiwa.

Vilevile matumizi ya neno **anafunguliwa** katika sentensi (3) limepotosha maana muafaka iliyokusudiwa kwani neno hilo linaonesha hali ya kutendewa badala ya hali ya kutendea **anamfungulia** ambalo ndilo lililokusudiwa katika sentensi hiyo.

Mwisho neno **kutembelewa** katika sentensi (4) linaashiria hali ya kutendwa badala ya hali ya kutendea ambayo ni **kutembelea** kama ilivyokusudiwa katika sentensi hali ambayo imepelekea kubadilika kwa maana iliyokusudiwa.

Maneno yote hayo, kama yanavyoonekana katika sentensi hapo juu, yanaonesha hali za kutenda na kutendwa badala ya hali ya kutendea ambayo imekusudiwa, hivyo hali hiyo imepelekea kukwamisha mawasiliano na maana iliyokusudiwa haikufikiwa.

Usahihi wa maneno hayo ni kama unavyoonekana hapo chini:

1. Kwa hivyo, watu wengi waliotoka Ujerumani Mashariki **walikimbilia** Ujerumani Magharibi
2. Samahani naomba posti kadi sita **kuwapelekea** rafiki zangu
3. Joyce **anamfungulia** John mlango.
4. Wakati wa jioni Lucas hupenda **kutembelea** Forodhani.

### 2.1.2 Hali ya kutenda

Katika aina hii ndogo ya makosa. Mwanafunzi ametumia hali za kutendeanana na kutendesha mahali pa hali ya kutenda, kwa mfano:

5. Rwanda kwa mfano **iliachisha** kuchukua misaada ya nguo za mitumba.

Katika sentensi (5) kumetumika neno **iliachisha** ambalo linaashiria hali ya kutendesha badala ya neno **iliacha** ambalo lipo katika hali ya kutenda hali ambayo imesababisha kutofikiwa kwa maana iliyokusudiwa. Usahihi wake ni kama ifuatavyo:

5. Rwanda kwa mfano **iliacha** kuchukua misaada ya nguo za mitumba.

### 2.1.3 Hali ya kutendwa

Katika aina hii ndogo ya makosa mwanafunzi ametumia hali za kutenda na kutendewa badala ya hali ya kutendwa kama inavyoonekana hapo chini:

6. Barua ambayo **ilipeleka**.....

7. Mlango huu **ulivunjiwa** na mtoto wangu.

Katika sentensi (6) mwanafunzi ameandika hali ya **kutenda** ilipeleka badala ya hali ya kutendwa ambayo ni **ilipelekwa** hali hiyo imekwaza maana.

Mwanafunzi katika sentensi (7) ametumia neno **ulivunjiwa** ambalo linaonesha hali ya kutendewa jambo ambalo limeathiri maana iliyokusudiwa. Neno sahihi lililopaswa kutumika ambalo linaonesha hali ya kutendwa ni **ulivunjwa**. Hivyo, sentensi hizo zilitakiwa ziandikwe:

6. Barua ambayo **ilipelekwa**.....

7. Mlango huu **ulivunjwa** na mtoto wangu.

## 2.2 Matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha wake

Katika aina hii ya makosa, wanafunzi wameweka msamiati ambao sio sahihi katika muktadha husika na hivyo husababisha kukwaza maana hasa iliyokusudiwa. Ifuatayo ni mifano ya sentensi ambayo ndani yake wanafunzi wametumia msamiati usiofaa kulingana na muktadha:

9. Lakini mama yangu ni mbaya na **hatuzungumzi** na mimi au kaka yangu.

10. Asingalikwenda Jozani **asingalioana** kima.

11. Halafu wanaweza kutumia taaluma zao kufanya kazi na **kuelewa** familia.

Mifano hiyo hapo juu inaonesha jinsi gani matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha wake ulivyokwamisha mawasiliano kwa kuleta maana isiyokusudiwa katika muktadha wa sentensi husika ambapo msamiati huo huo iwapo utatumika katika muktadha wake unaweza kuleta maana sahihi kwani msamiati huo upo na unatumika katika lugha ya Kiswahili, mfano:

Katika sentensi (9) mwanafunzi ametumia msamiati **hatuzungumzi** msamiati ambao unatokana na neno **zungumza** ambalo ni kitenzi ambacho kinaonesha hali ya wakati uliopo kanushi ambalo linaashiria nafsi ya pili wingi limewekwa mahali ambapo si pake kwa mujibu wa muktadha wa

sentensi husika hali ambayo inapotosha maana iliyokusudiwa. Neno sahihi lililopaswa kutumiwa ni neno **hazungumzi** ambalo linaonesha nafsi ya tatu umoja katika hali ya wakati uliopo kanushi kwani sentensi hiyo inamzungumzia mtu ambaye hayupo kupitia nafsi ya tatu umoja.

Katika sentensi (10) matumizi ya msamiati **kuoana** badala ya msamiati **kuona** ambao unatokana na neno **oa** msamiati huo upo na unatumika katika lugha ya Kiswahili ambao kwa mujibu wa Kamusi Pevu ya Kiswahili (2018) una maana ya:

<sup>1</sup>ungana na mwanamke kuishi naye katika ndoa kufuatana na mila, sheria, dini na kuishi mahali fulani; funga akidi, funga ndoa.

<sup>2</sup>oteza karata ya dume kwenye karata mke hasa katika mchezo wa karata.

Kutoka katika sentensi (11) neno **kuelewa** limetumiwa badala ya neno **kulea** maneno haya mawili yana maana tafauti na kulitumia neno moja mahali pa neno jengine ni kupotosha maana iliyokusudiwa kwani neno **kuelewa** kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Fasaha (2010) lina maana ya kitendo cha kufahamikiwa na jambo, na neno **kulea** maana yake kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha ni kitendo cha mtu kupewa dhamana ya utunzaji na ukuzaji wa mtu mwingine hasa mtoto.

Usahihi wa sentensi hizo ni kama inavyooneshwa hapa chini:

9. Lakini mama yangu ni mbaya na **hazungumzi** na mimi wala kaka yangu.
10. Asingalikwenda Jozani **asingaliwaona** kima.
11. Halafu wanaweza kutumia taaluma zao na **kulea** familia.

### 2.3 Udondoshaji wa kitamkwa katika neno

Katika hali hii iwapo kutakuwa na udondoshaji wa kitamkwa katika neno fulani, neno hilo hupoteza maana iliyokusudiwa kama inavyoonekana katika mifano:

12. Rafiki yangu ni **karimu** sana.
13. Biashara **imefunga** katika ramadhani.
14. **Anajaa** sana, akale chakula.

Sentensi (12) mwanafunzi amedondosha kitamkwa /m/ katika neno **karimu** badala ya neno **mkarimu**, udondoshaji huo umepelekea kupotosha maana iliyokusudiwa kwani hata aina ya neno lenyewe imebadilika kutoka aina moja kwenda nyengine. Neno karimu ni nomino na mkarimu ni kivumishi.

Katika sentensi (13) mwanafunzi amefanya udondoshaji wa kitamkwa /w/ katika neno **imefungwa**, hali hiyo imesababisha kukwamisha maana iliyokusudiwa, maneno imefunga na imefungwa ni maneno yenye asili zinazofanana lakini zina utafauti katika matumizi na utafauti huo ndio unaopelekea kubadili maana.

Na katika sentensi (14) kumetokea udondoshaji wa kitamkwa /n/ katika neno ana **njaa**, udondoshaji huo umeharibu maana kwani neno **njaa** na neno **jaa** ni maneno mawili yenye tafsiri tafauti kwani neno **jaa** kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu lina maana ya:

<sup>1</sup>kuwa tele; tapakaa kila mahali; kuwa na maungo makubwa.

---

**Makosa ya Kisemantiki Katika Maandishi ya Wanafunzi Wageni  
Wanaojifunza Lugha ya Kiswahili, Mwanaidi Juma Jaku**

---

<sup>2</sup> mahali pa kutupia taka; mtu mzima au mwenye cheo hupata habari nyingi za watu wa chini yake. Na neno njaa maana yake kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2014) ni:

<sup>1</sup> hali ya mtu kujisikia kuwa anahitaji chakula.

<sup>2</sup> ukosefu mkubwa wa chakula.

Hivyo, udondoshaji wa vitamkwa vyote hivyo katika sentensi hizo umesababisha kupotea kwa maana iliyokusudiwa, na usahihi wa sentensi hizo ambao ndio unaashiria maana halisi iliyokusudiwa ni:

12. Rafiki yangu ni **mkarimu** sana.

13. Biashara **imefungwa** katika mwezi wa ramadhani.

14. Ana **njaa** sana, akale chakula.

#### 2.4 Tafsiri sisizi

Miongoni mwa makosa makubwa yanayofanywa na wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili ni makosa ya tafsiri sisizi (ambayo ni tafsiri ya neno kwa neno). Hali hii hupelekea kupotea kwa maana iliyokusudiwa, ambapo wanafunzi walitafsiri maneno ya lugha ya Kiswahili kwa kutumia tafsiri ya moja kwa moja kutoka katika lugha zao za awali kama inavyohibitishwa katika sentensi zifuatazo:

15. Na hawapendi **kuuliza** wengine msaada.

16. Wanawake wanapaswa **kutibiwa** kwa heshima.

17. Kila siku ninapoamka **ninafanya** kahawa.

18. Ni bora unywe maji **joto** pamoja na ndimu.

19. Wanafunzi wengi walifanya **uchunguzi**.

20. ....ninaweka **begi la chai** katika chupa.

Athari ya tafsiri ya neno kwa neno inaweza kuonekana iwapo neno litatafsiriwa visivyo kutoka katika lugha moja kwenda lugha nyengine, athari hiyo ni kama inavyoonekana katika sentensi hizo hapo juu ambapo maana halisi iliyokusudiwa haikufikiwa.

Katika sentensi (15) mwanafunzi ametumia neno **kuuliza** kama ni tafsiri ya neno *ask* neno ambalo katika lugha ya Kiingereza lina maana ya **kuomba** au **kuuliza**, lakini kwa mujibu wa muktadha wa sentensi neno muafaka lililotakiwa kutumika ni neno **kuomba**.

Vilevile katika sentensi (16), neno **kutibiwa** limetumiwa na mwanafunzi kama ni tafsiri ya neno la Kiingereza *treated* ambalo lina maana ya kutibiwa au kutunzwa, lakini katika muktadha wa sentensi hiyo neno **kutunzwa** ndilo hasa lingetakiwa kutumika.

Katika sentensi (17) mwanafunzi ametumia neno **ninafanya** kama ni mbadala wa neno **ninapika**, hii inatokana na tafsiri ya moja kwa moja ya neno make katika lugha ya Kiingereza hali ambayo imesababisha kupotosha maana iliyokusudiwa.

Mwanafunzi katika sentensi (18) amelitafsiri neno *hot* la Kiingereza kwa kuweka neno joto badala ya neno **yamoto**, hali ambayo imesababisha kupotea kwa maana halisi.

---

Sentensi (19) mwanafunzi ametumia neno **uchunguzi**. Katika sentensi hiyo neno hilo limetumiwa kama ni tafsiri ya neno **examinations** hali ambayo imeondosha maana iliyokusudiwa kwani kwa mujibu wa sentensi hiyo neno **examinations** lilitakiwa litafsrike kama **mitihani** na sio uchunguzi kama lilivyotafsiriwa.

Na sentensi (20) maneno **begi la chai** yametumiwa ikiwa ni tafsiri ya maneno **tea bag** kutoka lugha ya Kiingereza, hali ambayo imepotosha maana iliyokusudiwa na maneno sahihi yaliyotakiwa kuandikwa hapo ni **majani ya chai**.

Kama inavyoonekana katika sentensi za hapo juu kutokana na matumizi ya tafsiri yasiyo sahihi, maana halisi iliyokusudiwa imepotea na hivyo kusababisha upotevu wa mawasiliano. Usahihi wa sentensi hizo ni kama inavyoonekana hapa chini:

15. Na hawapendi **kuomba** wengine msaada.
16. Wanawake wanapaswa **kutunzwa** kwa heshima.
17. Kila siku ninapoamka **ninapika** kahawa.
18. Ni bora unywe maji **yamoto** pamoja na ndimu.
19. Wanafunzi wengi walifanya **mitihani**.
20. Ninaweka **majani ya chai** katika chupa.

### 2.5 Kubadili mpangilio wa fonimu

Katika kila lugha kunakuwa na utaratibu maalumu wa upangaji wa fonimu katika neno ili neno hilo liweze kutoa maana na kufikisha ujumbe uliokusudiwa, kinyume na hivyo mpangilio usio sahihi wa fonimu hizo katika neno huchangia upotevu wa maana iliyokusudiwa. Mfano:

21. Wao hupiga **pisa** kila jioni.

Katika sentensi (21) inaonekana kuwa neno **pisa** limetumika kama ni mbadala wa neno **pasi** hali ambayo imeleta mkanganyiko katika maana iliyokusudiwa kwani maneno hayo ni yenye maana tafauti. Usahihi wa sentensi hiyo ni:

21. Wao hupiga **pasi** kila jioni.

### 2.6 Udondoshaji wa maneno katika sentensi

Kila lugha duniani ina utaratibu wake wa uundaji wa sentensi, katika lugha ya Kiswahili kwa mfano vipo viambajengo mbalimbali vinavyotumika kuunda sentensi na ikaleta maana, hivyo udondoshaji wa kiambajengo kimojawapo cha sentensi ukitokea sentensi hiyo hupoteza maana iliyokusudiwa na hivyo hukwamisha mawasiliano.

22. **Mwanafunzi - Kiswahili** alikuwa hapa.
23. Nitaposoma **kitabu - Kiingereza**
24. Wao huenda Europe **mwezi - kumi na moja** kila mwaka
25. **Mwalimu - Kiswahili** alikuwa hapa

Katika sentensi (22 na 25) umetokea udondoshaji wa neno **wa**, neno ambalo lilipaswa kuwepo baina ya maneno mwanafunzi na Kiswahili (22) na mwalimu na Kiswahili (25), hali hiyo imesababisha

---



kuleta maana tafauti ambapo kwa mujibu wa sentensi hizo maana ambayo itapatikana ni Kiswahili ni jina la mwanafunzi au mwalimu maana ambayo siyo iliyokusudiwa.

Katika sentensi (23) mwanafunzi amedondosha neno **cha**, neno ambalo mahali pake ni baina ya maneno kitabu na Kiingereza, udondoshaji huo umepelekea kupoteza maana iliyokusudiwa ambapo kwa mujibu wa sentensi ilivyo maana itakayopatikana ni kuwa jina la kitabu ni Kiingereza na sio aina ya kitabu hali ambayo imepoteza maana iliyotakiwa imfikie msomaji.

Vilevile katika sentensi (24) neno **wa** limedondoshwa na hivyo kusababisha upotevu wa maana ambapo sentensi hiyo itakuwa na maana ya siku ya mwezi kumi na moja kama ambavyo inatumiwa na Waswahili na sio mwezi kama ilivyokusudiwa.

### 2.7 Kutenganisha maneno mahali pasipostahiki

Kutenganisha maneno mahali pasipostahiki ni kosa katika lugha ya Kiswahili kwani huleta athari ya moja kwa moja kwa kutofikiwa maana iliyokusudiwa kama inavyoonekana katika sentensi zifuatazo:

26. Wewe **huku-sikiliza** redio

27. Watoto **wana-piga** picha

28. Je wazazi wako wana ndege ya abiria? Hapana, wazazi wangu **hawa-na** ndege ya abiria

29. Mimi **siku-lala** vizuri.

Sentensi hizi zinaonesha jinsi gani kutenganisha maneno kunaweza kukwamisha mawasiliano, kwa kufanya hivyo kunasababisha kutoweka kwa maana iliyokusudiwa na hivyo kuleta maana nyengine isiyokusudiwa. Maneno hayo sio kwamba hayapatikani au hayana maana katika lugha ya Kiswahili lakini kutenganishwa kwake ndiko kulikopotosha maana iliyokusudiwa.

Katika sentensi (26) neno **hukusikiliza** lilitenganishwa ambalo chanzo chake ni kitenzi lakini baada ya kutenganishwa limebadili uasili wake na kubadili maana kwa ujumla, mfano neno “huku” ni kivumishi kioneshi cha mahali na neno “sikiliza” ni kitenzi ambacho kwa mujibu wa Kamusi Pevu ya Kiswahili (2018) lina maana ya kufuata ushauri au maelekezo, hivyo haya ni maneno mawili yenye maana tafauti.

Sentensi (27) neno **wanapiga** ni kitenzi lakini kutokana na kutenganishwa kwake limeleta maana nyengine ambapo neno “wana” ambalo ni wingi wa neno mwana lina maana ya mtoto wa mtu au mnyama (hii ni kwa mujibu wa Kamusi la Kiswahili Fasaha (2010)).

Pia sentensi (28) neno **hawana**, neno hawa linaashiria kivumishi au kiwakilishi kioneshi na neno na linaweza kusimama kama kiunganishi.

Sentensi (29) mwanafunzi ametenganisha neno **sikulala** na kuwa maneno mawili siku na lala hali ambayo imechangia kupotea kwa maana iliyokusudiwa kwani kutenganishwa huko si katika utaratibu wa utenganishaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili.



Ufuatao ni usahihi wa maneno hayo kama yanavyotumika katika lugha ya Kiswahili:

26. Wewe **hukusikiliza** redio
27. Wao **wanapiga** picha
28. Je wazazi wako wana ndege ya abiria? Hapana, wazazi wangu **hawana** ndege ya abiria
29. Mimi **sikulala** vizuri.

### 2.8 Kuunganisha maneno

Kuunganisha maneno ni katika makosa makubwa yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni. Hali hii husababisha kupotea kwa maana hasa iliyokusudiwa katika muktadha husika kwani si maneno yote yanayunganishwa na kuleta maana, ingawa yapo baadhi yao kutokana na muundo wake ni lazima yaunganishwe ili kukamilisha maana, maneno hayo katika lugha ya Kiswahili huitwa maneno ambatano. Mfano wake ni maneno kama mwanajeshi, batamzinga, miundombinu, mfanyabiashara, gugumaji, pandungozi na mengineyo. Sentensi zifuatazo zina maneno yaliyounganishwa na hivyo kupoteza maana halisi iliyokusudiwa:

30. **Hikini** chako kitabu.
31. **Hikini** chumba changu.

Katika sentensi hizo inaonesha kuwa kuunganishwa kwa maneno hayo kumepoteza taswira na maana halisi iliyokusudiwa katika sentensi hizo kwani inaonekana kwamba asili ya maneno hayo si kuunganishwa bali ni kutenganishwa ili yaweze kuleta maana, hali hiyo inaweza kumchanganya msomaji na asifikie lile lengo lililokusudiwa na mwandishi.

Mfano katika sentensi (30 na 31) zimeandikwa **hikini** kuashiria maneno mawili **hiki** na **ni**.

Sentensi hizo zimesahihishwa kama ifuatavyo:

32. **Hiki ni** kitabu chako.
33. **Hiki ni** chumba changu.

### 3.0 Vyanzo vya makosa ya kisemantiki

Vyanzo hivi ni kwa mujibu wa maoni ya walimu kupitia usaili uliofanywa na mwandishi kwa walimu, ambapo imebainika kuwa vyanzo vya makosa ya kisemantiki katika maandishi ya wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili ni athari za lugha ya kwanza, ugumu wa sheria za lugha ya pili na pia ukosefu wa mazoezi miongoni mwa wanafunzi.

Aladin, Darus na Rajab (2016) wameandika kuhusu uchunguzi wa makosa ya kisemantiki katika maandishi kwa wanafunzi wa Libya wanaojifunza Kiingereza kama lugha ya kigeni na wamegundua kuwa chanzo cha makosa hayo ni athari ya lugha mama au ugumu wa lugha ya pili.

Al- Shohbani na Al- Shormani (2012) walifanya utafiti kuhusu makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Yemen: Mgawanyo na vyanzo. Katika utafiti huo wamebaini kuwa vyanzo vya makosa hayo ni athari ya lugha mama na ugumu wa lugha ya pili.

Nao Jeptarus na Ngene (2016) wamefanya utafiti kuhusu makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wa darasa la saba wanaozungumza lugha ya Keiyo wanapojifunza Kiswahili, na

---

## Makosa ya Kisemantiki Katika Maandishi ya Wanafunzi Wageni Wanaojifunza Lugha ya Kiswahili, Mwanaidi Juma Jaku

---

wamebaini kuwa sababu za makosa hayo ni muingiliano wa lugha ya kwanza na ugumu uliopo katika sheria za lugha ya pili.

### 3.1 Athari za lugha ya kwanza

Kwa kawaida katika kitendo cha kujifunza lugha ya pili makosa yanaweza kujitokeza, makosa hayo husababishwa na athari za lugha ya kwanza ya mwanafunzi kwani katika hatua za awali mwanafunzi huwa na uchache wa msamiati na hivyo hulazimika kuingiza uzoefu alionao kutoka lugha yake ya awali katika lugha anayojifunza.

Hanna (1986) anaeleza kuwa sababu za makosa ya athari za lugha ya kwanza ni katika kuzidisha jumla, ukakamaaji, na urahisishaji.

Richards (1970) anaeleza kuwa sababu za makosa ya athari za lugha ya kwanza zimegawika katika vipengele vya kuzidisha jumla, dhana za uongo, ukakamaaji na marekebisho makubwa.

Kufuatia usaili wa walimu tafauti, mtafiti amegundua kwamba yapo makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama lugha ya kigeni ambayo chanzo chake ni athari za lugha ya kwanza kama inavyoonekana hapo chini:

#### 3.1.1 Kuzidisha jumla

Hii ni hali ambayo mwanafunzi hutumia ujuzi alionao kutoka lugha yake ya awali katika kujifunza lugha ya pili. Mfano katika makosa ya tafsiri sisizi kama inavyooneshwa katika mifano ifuatayo:

15. Na hawapendi **kuuliza** wengine msaada.
16. Wanawake wanapaswa **kutibiwa** kwa heshima.
17. Kila siku ninapoamka **ninafanya** kahawa.
18. Ni bora unywe maji **joto** pamoja na ndimu.
19. Wanafunzi wengi walifanya **uchunguzi**.
20. ....ninaweka **begi la chai** katika chupa.

Katika sentensi (15-20) mwanafunzi ametafsiri maneno isivyo sahihi na hivyo kupotosha maana.

Usahihi wa sentensi hizo ni kama inavyoonekana hapa chini:

15. Na hawapendi **kuomba** wengine msaada.
16. Wanawake wanapaswa **kutunzwa** kwa heshima.
17. Kila siku ninapoamka **ninapika** kahawa.
18. Ni bora unywe maji **yamoto** pamoja na ndimu.
19. Wanafunzi wengi walifanya **mitihani**.
20. Ninaweka **majani ya chai** katika chupa.

### 3.2 Ugumu wa lugha ya pili

Hanna (1986) anafafanua kuwa sababu ya ugumu wa lugha ya pili katika kujifunza lugha inatokana na mambo yafuatayo; kuepuka, na elimu duni ya lugha ya pili.

Nae Richards (1970) anaeleza kuwa makosa yanayotokana na ugumu wa lugha ya pili ni pamoja na kutokujua kizuizi cha sheria za lugha ya pili.

Mahojiano ya walimu yaliyofanywa na mtafiti yameonesha kuwa zipo sababu zinazotokana na ugumu wa lugha ya pili ambazo ni pamoja na:

### 3.2.1 Kuepuka

Kufuatia ugumu wa baadhi ya maumbo ya kisintaksia kwa baadhi ya wanafunzi, mwanafunzi huepuka kutumia maumbo hayo, mfano huo unaonekana kupitia makosa ya udondoshaji wa kitamkwa katika neno na udondoshaji wa maneno katika sentensi kama inavyoonekana hapa chini kwa kuanza na udondoshaji wa kitamkwa katika neno:

12. Rafiki yangu ni **karimu** sana.
13. Biashara **imefunga** katika ramadhani.
14. **Anajaa** sana, akale chakula.

Kama inavyoonekana katika sentensi (12-14) katika mifano, kumekuwa na udondoshaji wa baadhi ya vitamkwa katika baadhi ya maneno hali hii imesababishwa na wanafunzi kuepuka kutamka baadhi ya vitamkwa katika neno jambo ambalo limepoteza maana halisi iliyokusudiwa. Usahihi wa sentensi hizo ni;

12. Rafiki yangu ni **mkarimu** sana.
13. Biashara **imefungwa** katika ramadhani.
14. Ana **njaa** sana, akale chakula.

### 3.2.2 Elimu duni katika lugha ya pili

Hii husababishwa na upungufu wa elimu ya lugha ya pili katika kujifunza lugha hiyo. Hali hii inaonekana katika kipengele cha matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha wake. Kwa vile mwanafunzi hajapata elimu ya kutosha kuhusu lugha ya pili, hivyo hushindwa kutumia msamiati muafaka kulingana na muktadha husika, kama inavyoonekana katika sentensi zifuatazo:

9. Lakini mama yangu ni mbaya na **hatuzungumzi** na mimi au kaka yangu.
10. Asingalikwenda Jozani **asingalioana** kima.
11. Halafu wanaweza kutumia taaluma zao kufanya kazi na **kuelewa** familia.

Sentensi (9-11) zinaonesha jinsi gani elimu duni katika lugha ya pili imesababisha matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha wake na hivyo yameathiri maana iliyokusudiwa. Ufuatao ni usahihi wa sentensi hizo.

9. Lakini mama yangu ni mbaya na **hazungumzi** na mimi wala kaka yangu.
  10. Asingalikwenda Jozani **asingaliwaona** kima.
-

---

**Makosa ya Kisemantiki Katika Maandishi ya Wanafunzi Wageni  
Wanaojifunza Lugha ya Kiswahili, Mwanaidi Juma Jaku**

---

11. Halafu wanaweza kutumia taaluma zao kufanya kazi na **kulea** familia zao.

### 3.2.3 Kutokujua kizuizi cha kanuni za lugha ya pili

Katika hali hii mwanafunzi anatumia kanuni kulingana na mazingira yake na sio sheria za lugha zinavyoruhusu. Hilo linajitokeza katika makosa yanayotokana na matumizi mabaya ya mnyambuliko wa hali za vitenzi, kutenganisha maneno, kuunganisha maneno na kubadili mpangilio wa fonimu. Kwa kuanza na makosa ya matumizi mabaya ya mnyambuliko wa hali za vitenzi kama inavyoonekana katika sentensi zifuatazo:

1. Kwa hivyo watu wengi waliotoka Ujerumani Mashariki **walikimbia** Ujerumani Magharibi.
2. Samahani naomba posti kadi sita **kupeleka** rafiki wangu.
3. Joyce **anafunguliwa** John mlango.
4. Wakati wa jioni Lucas hupenda **kutembelewa** Forodhani.

Kama inavyoonekana katika sentensi (1- 4) kumetumika hali za kutenda na kutendewa badala ya hali ya kutendea hali ambayo imesababishwa kukiuka sheria za lugha ya pili hali ambayo imeathiri maana iliyokusudiwa.

Usahihi wa sentensi hizo ni kama ifuatavyo:

1. Kwa hivyo, watu wengi wanaotoka Ujerumani Mashariki **walikimbilia** Ujerumani Magharibi.
2. Samahani naomba postikadi sita **kuwapelekea** rafiki zangu.
3. Joyce **anamfungulia** John mlango.
4. Wakati wa jioni Lucas hupenda **kutembelea** Forodhani.

### Makosa ya hali ya kutenda

5. Rwanda kwa mfano **iliachisha** kuchukua misaada ya nguo za mitumba

Katika sentensi (5) mwanafunzi ametumia hali ya kutendesha mahali pa hali ya kutenda hali ambayo imepotosha maana.

Sentensi ilitakiwa isomeke kama ifuatavyo:

5. Rwanda kwa mfano **iliacha** kuchukua nguo za mitumba.

### Makosa ya hali ya kutendwa

6. Barua ambayo **ilipeleka**.....
7. Mlango huu **ulivunjiwa** na mtoto wangu.

Katika sentensi (6) mwanafunzi ametumia hali za kutendeka badala ya hali ya kutendwa, hivyo kufanya maana iliyokusudiwa isipatikane.

Neno ulivunjiwa ambalo ni hali ya kutendea katika sentensi (7) limesababisha kutofahamika kwa maana iliyokusudiwa kwa sababu limetumika mahali pasipostahiki.

Ufuatao ni usahihi wa sentensi hizo:

6. Barua ambayo **ilipelekwa**.....

7. Mlango huu **ulivunjwa** na mtoto wangu.

Kwa kuendelea, makosa ya kutenganisha maneno pasipostahiki yamejitokeza kama ifuatavyo:

26. Wewe **huku-sikiliza** redio

27. Watoto **wana-piga** picha

28. Je wazazi wako wana ndege ya abiria? Hapana, wazazi wangu **hawa- na** ndege ya abiria.

29. Mimi **siku-lala** vizuri

Kama inavyoonekana katika sentensi hapo juu (26-29) kumetokea utenganishaji wa maneno pasipostahiki na hivyo kusababisha kupotea kwa maana. Usahihi wa sentensi hizo ni:

26. Wewe **hukusikiliza** redio.

27. Watoto **wanapiga** picha.

28. Je wazazi wako wana ndege ya abiria? Hapana, wazazi wangu **hawana** ndege ya abiria.

29. Mimi **sikulala** vizuri.

Kwa kuongezea, pia yapo makosa ya kuunganisha maneno kama ifuatavyo:

30. **Hikini** chako kitabu.

31. **Hikini** chumba changu.

Katika sentensi (30-31) maneno hayo yameunganishwa hali ambayo ni kinyume na sheria za lugha na hivyo kupotosha maana iliyolengwa.

Sentensi hizo zinasahihishwa kama ifuatavyo:

30. **Hiki ni** chako kitabu.

31. **Hiki ni** chumba changu.

Makosa mengine yaliyojitokeza katika sababu hii ni makosa ya kubadili mpangilio wa fonimu kama inavyoonekana katika sentensi ifuatavyo:

21. Wao hupiga **pisa** kila jioni

Katika sentensi (21) kama inavyoonekana hapo juu inaonesha jinsi gani mpangilio mbaya wa fonimu ulivyosababisha kupotosha maana iliyokusudiwa. Usahihi wake ni kama unavyoonekana hapa chini:

---

21. Wao hupiga **pasi** kila jioni.

### **3.3 Ukosefu wa mazoezi miongoni mwa wanafunzi**

Hii ni miongoni mwa sababu zilizogunduliwa na mtafiti kutoka kwa watoa taarifa, sababu hii inatokana na mwanafunzi mwenyewe binafsi, ambapo wameeleza kuwa kutokufanya mazoezi kwa kile ambacho wamefundishwa darasani kunapelekea kutokea mara kwa mara kwa makosa ya kisemantiki kwa wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili, (kama inavyoonekana katika sentensi 1-31) kwani inaaminika kuwa wapo baadhi ya wanafunzi hawashirikiani na wazawa wa lugha ya Kiswahili katika kufanya mazoezi ya kuzungumza au kuandika na hivyo kupelekea kufanya makosa hayo. Kama inavyofahamika kuwa, katika kujifunza lugha ya pili au zaidi mazoezi kwa kuchanganyika na wazawa wa lugha husika ni kitu muhimu na ndio yanayomfanya mwanafunzi kuepukana na kutenda makosa mbalimbali yakiwemo makosa ya kisemantiki na hivyo kumsaidia kukuza kiwango chake cha ujifunzaji wa lugha.

### **4.0 Mapendekezo**

Kwanza, mwalimu anashauriwa kurudia msamiati mara kwa mara ili kumfanya mwanafunzi kuukumbuka msamiati huo na hivyo kujua msamiati sahihi wa kuutumia katika muktadha husika. Pili, mwalimu anashauriwa kumuuliza mwanafunzi maswali mengi ili kuweza kujua changamoto inayomkabili mwanafunzi hasa katika kipengele cha upungufu wa msamiati. Aidha, inapendekezwa mwalimu kutoa mbadala wa neno fulani na kufundisha maana ya ziada ya neno hilo na kufafanua matumizi ya kila neno ili kuepusha matumizi ya msamiati usiofaa katika muktadha. Mwisho, mwalimu anashauriwa kutumia njia za vikundi katika ufundishaji wake ili ikitokea wapo baadhi ya wanafunzi wenye changamoto katika eneo fulani waweze kusaidiana wenyewe kwa wenyewe.

Kwa upande wa wanafunzi, inashauriwa kuwa mazoezi ya kutosha yanahitajika hasa na wazawa wa lugha katika mchakato mzima wa kujifunza lugha hasa ya Kiswahili kwani mazoezi hayo yatawasaidia kuondokana na makosa ya kisemantiki yanayojitokeza wakati wanapojifunza.

### **5.0 Hitimisho**

Kwa ujumla imebainika kuwa makosa ya matumizi mabaya ya kauli za vitenzi ni makosa yanayofanywa zaidi na wanafunzi wageni wanaojifunza lugha ya Kiswahili. Hivyo, walimu wanaofundisha Kiswahili kwa wanafunzi wageni, wanashauriwa kuzidisha umakini hasa katika aina hii ya makosa, ingawa makosa ya mpangilio mabaya wa fonimu ni makosa yanayojitokeza kwa uchache miongoni mwa wanafunzi hao. Kwa upande wa sababu imeonekana kuwa athari ya lugha ya kwanza, ugumu wa sheria za lugha ya pili na ukosefu wa mazoezi miongoni mwa wanafunzi ni sababu zinazopelekea kutokea kwa makosa hayo.

**Marejeo**

- Ahmed, M. & Zribi, C. (2013). Detection of semantic errors in Arabic texts. *Artificial*
- Al Shohbani, Y. & Al Shormani, M. (2012). Semantic errors committed by Yemeni University learners: Classifications and sources. *Internationa Journal of English Linguistics*. 2,6.
- Aladin, A., Darus, S & Rajab, A. (2016). An Investigation of semantic interlingual errors in the writings of Libyan English as a foreign language learners. *Arab World English Journal*. 7, 4, 277-292.
- Aruba, B. (2017). *Makosa ya kisemantiki katika mawasiliano andishi ya Kiswahili miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili: Mfano kaunti ya Kakamega (Tasnifu ya Uzamili*. Chuo Kikuu Maasai Mara.
- BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili fasaha*. Oxford University Press.
- Corder, S. (1987). *Error analysis and interlanguages*. Oxford University Press.
- Hanna, Y. (1986). Second language learning errors, their types, causes and treatment. *JALT Journal*. 8,1.
- Jeptarus, K. & Ngene, K. (2016). Lexico-semantic errors of the learners of English: A survey of standard seven Keiyo-speaking primary school pupils. *Journal of Education and Practice*. 7,13.
- Kroeger, P. (2019). *Analysing meaning. An introduction to semantics and pragmatics*. Language science Press.
- Leena, J. (2016). An analysis of semantic errors in Iraq EFL learners' writings. *Journal of Thi-Qar University*. 11,4.
- Richards, J. (1974). *Error analysis and second language strategies*. Longman.
- TUKI. (2014). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press.
- Wamitila, K. W. (2018). *Kamusi pevu ya Kiswahili*. Vide-Muwa Publishers Limited.
- [www.suza.ac.tz/school-of-kiswahili-foreignlanguage-skfl/](http://www.suza.ac.tz/school-of-kiswahili-foreignlanguage-skfl/)
- [www.udsm.ac.tz/thecentre-for-kiswahili-for-foreigners](http://www.udsm.ac.tz/thecentre-for-kiswahili-for-foreigners)